JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la 12

# BAJETI

## *ya Kuimarisha Utoaji Haki*

- Bunge laidhinisha **441.2b**




***Bodi ya Uhariri***

**Bi Mary Makondo**
KATIBU MKUU

**Lusajo Mwakabuku**
MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO CHA SERIKALI

William Mabusi
Hyasinta Kissima
Waziri Bosco
Ibrahim Joseph


# BAJETI YA KUIMARISHA MIFUMO YA UTOAJI HAKI KWA WOTE



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akisoma Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025*

**Na Hyasinta Kissima & William Mabusi**
**-** WKS DODOMA

Wizara ya Katiba na Sheria imepanga kutumia jumla ya Shilingi Bilioni 441.26 kwa mwaka wa fedha 2024/25 huku vipaumbele vikijikita katika uimarishaji wa huduma za Sheria na utoaji wa haki kwa umma.




Akisoma Bajeti hiyo, Bungeni Jijini Dodoma Aprili 29, 2024 Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alisema Wizara na Taasisi zake itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za Sheria na utoaji wa haki kwa umma kutumia kampeni mbalimbali ikiwemo Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, kutoa elimu kwa jamii kuhusu mchakato wa Katiba mpya, kufanya marekebisho ya Sheria, na kuendelea kuimarisha mifumo ya utoaji haki.

Katika hotuba yake Dkt. Pindi Chana amesema kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/25 Wizara na Taasisi zake zitaendelea na utoaji wa elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma. Wizara imepanga kuendelea kutoa elimu kwa Wananchi ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuanza mchakato wa Katiba Mpya ili kuendelea kuimarisha Demokrasia katika Nchi.

Kuboresha utoaji wa huduma za Sheria na utoaji wa haki kwa umma ili kuendana na Mipango ya Sekta ya Sheria nchini na Mipango ya Kikanda na Kimataifa ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

Kuendelea kuratibu na kusimamia masuala ya upatikanaji wa huduma za msaada wa Kisheria kwa Wananchi kote Nchini kupitia Kampeni mbalimbali ikiwemo Kampeni ya Msaada wa Kisheria wYa Mama Samia.

Kusimamia Mfumo wa Haki na Utoaji Haki kwa kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Haki Jinai,kufanya mapitio ya Sheria ya kuwalinda watoa Taarifa na Mashahidi ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoa taarifa na mashahidi unaimarishwa.

Kuendelea kuimarisha mfumo wa uangalizi wa utajiri asili na maliasili za Nchi. Wizara imepitia mikataba 18 ya kukuza na kulinda uwekezaji kati ya Tanzania na Nchi mbalimbali kwa lengo la kubaini iwapo inakidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria Nchini ikiwa ni pamojanamifumoyahudumazamahakama kwa njia ya kielektroniki ili kupunguza mrundikano wa mashauri mahakamani.

# VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

(1) Kutunga **Sera ya Taifa ya Haki Jinai**;

(ii) Kushughulikia masuala ya kikatiba ikiwa ni pamoja na kutoa **elimu ya Katiba na Uraia kwa Umma**;

(iii) Kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki ikiwa ni pamoja na kuimarisha **miundombinu ya Mahakama,** kuharakisha mashauri ya kawaida na kumaliza **mashauri ya muda mrefu**;

(iv) Uandishi wa sheria ikiwa ni pamoja na Kuandaa **Toleo la Sheria Ndogo zilizofanyiwa urekebu mwaka 2025** na kuimarisha Marejeo na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mikataba iliyosainiwa;

(v) Kuendesha mashtaka ya jinai Kuimarisha **utenganishaji wa shughuli za Mashtaka na Upelelez**i;

(vi) Kushughulikia uendeshaji wa mashauri ya madai na **usuluhishi wa migogoro ya kibiashara,** sheria za kimataifa na mikataba;

(vii) Kuwezesha uanzishwaji wa **Kituo cha Usuluhishi wa Migogoro;**

(viii) Kuwezesha **Ofisi ya Mwandishi Mkuu** wa Sheria kuanza kutekeleza majukumu;

(ix) Kuratibu masuala ya **haki za binadamu, utawala bora** na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa **kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia;**

(x) Kuimarisha **usajili wa matukio muhimu ya binadamu** pamoja na usajili na ufilisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara;

(xi) Kuratibu tathmini na maboresho ya sheria ikiwa ni pamoja na Kufanya **Mapitio ya Mifumo wa Sheria** inayosimamia Elimu, Michezo ya Kubahatisha, **Adhabu ya kifo na Kifungo cha Maisha**;

(xii) Kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya **utekelezaji wa sheria za utajiri asili na maliasilia za nchi;**

(xiii) Kushughulikia **urejeshwaji wa wahalifu** na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwenye makosa ya jinai;

(xiv) Kuimarisha **matumizi ya TEHAMA** katika utoaji haki na huduma za kisheria;

(xv) Kuboresha utendaji na maendeleo ya **rasilimali watu ya Wizara na taasisi zake.**



*Jengo la Vituo sita Jumuishi vya Utoaji Haki (Integrated Justice Cen-tres) liliopo Jijini Dodoma.*

# Serikali Kuendelea Kukisaidia Chama cha Msalaba Mwekundu



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko akihutubia kwenye Maadhimisho ya Miaka 62 ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mei 11, 2024 Jijini Dodoma.*

**Na William Mabusi**
- WKS DODOMA

Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dotto Biteko na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana wamesema Serikali itaendelea kukiwezesha Chama cha Msalaba Mwekundu nchini kutoa huduma za uokozi kwa wananchi wanaopatwa na madhira ama changamoto mbalimbali zinazoathiri maisha yao. Kauli hiyo imetolewa kwa nyakati tofauti wakati viongozi hao wakihutubia kwenye kilele cha Maadhimisho ya miaka 62 ya Chama cha Msalaba Mwekundu nchini Mei 11, 2024 Jijini Dodoma.

Maadhimisho hayo yamefanyika Kitaifa katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete na kuhudhuriwa na mamia ya wanachama wa Taasisi hiyo kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar yakibeba kauli mbiu isemaya "Natoa kwa furaha na furaha ninayotoa ni zawadi."

"Ninyi huwa mstari wa mbele na kuhatarisha uhai wenu kwa kuokoa maisha ya watu wengine, kwa kufanya hivyo mnaisaidia Serikali katika utoaji wa huduma za kibinadamu kwa wahanga wa majanga mbalimbali, Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Red Cross katika mazingira yote hata ya furaha." Amesema Dkt. Biteko huku akimtaka Rais wa Chama cha Msalaba Mwekundu nchini Mhe. David Kihenzile kuendelea kuwasajili vijana kuongeza wanachama kwenye Chama hicho.

Naye Dkt. Chana akiongea kwenye maadhimisho hayo amesema "Wizara itaendelea kuweka kanuni na miongozo mbalimbali kuhakikisha Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania kinatimiza majukumu yake nchini. Aidha, Serikali itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Red Cross kuhakikisha Wananchi wanaopatwa na madhira na changamoto mbalimbali zinazoathiri

maisha yao wanahudumiwa kwa wakati."

Awali akimkaribisha Mgeni Rasmi Rais wa Chama cha Msalaba Mwekundu nchini na Naibu Waziri wa Uchukuzi Mhe. David Kihenzile amesema kwa sasa Red Cross ina Matawi 1600 Tanzania Bara na Zanzibar ikiwa na wanachama zaidi ya laki 6. Aidha, aliongeza kuwa Red Cross imo mbioni kujenga ofisi mpya kwenye mikoa 12 na kwamba ina mpango wa kujenga nyumba 35 kwa Watanzania waliobomolewa nyumba zao Wilayani Hanang'.

Katika Maadhimisho hayo Rais wa Jamhuriya Muunganowa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye Kikatiba ndiye Mlezi wa Jumuiya hiyo ambaye aliwakilishwa na Naibu Waziri Mkuu Mhe. Dkt. Dotto Biteko alitunikiwa Tuzo Maalum ya Ubinadamu ikiwa ni tuzo ya pili kutolewa hapa nchini, Tuzo kama hiyo iliwahi kutolewa kwa Baba wa Taifa hayati Mwl. Julius Nyerere.



*Mgeni Rasmi akiwa na baadhi ya viongozi wakifuatilia matukio mbalimbali yaliyoambatana na Maadhimisho ya Miaka 62 ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mei 11, 2024 Jijini Dodoma.*



# MHE. SAGINI

## KARIBU

# MoCLA!



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akimkabidhi Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini vitendea kazi baada ya kupokelewa Wizarani Mtumba, tarehe 08 Aprili, 2024.*

**Na William Mabusi**
- WKS DODOMA

Naibu Waziri mpya wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini amestushwa na mapokezi makubwa yaliyofanywa na Viongozi wa Wizara hiyo pamoja na Watumishi na kukiri kuwa hiyo ni mara yake ya kwanza kukutana na mapokezi makubwa kiasi hicho.

Mhe. Sagini ameyasema hayo wakati akiongea na Watumishi wa Wizara hiyo alipopokelewa kwa mara ya kwanza Wizarani hapo tarehe 8 Aprili, 2024 baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

"Haya ni mapokezi ambayo nilikowahi kupita sijawahi kukutana nayo, lakini Wizara ya Katiba na Sheria mko vizuri sana, napokea mapokezo hayo kama ishara ya mahusiano mema, ambacho ni kitu kizuri kwenye utumishi wa umma katika kufikia malengo ya taasisi."

Mhe. Sagini amesisitiza upendo mahala pa kazi huku akionya kwamba kufanya kazi kwa upendo haina maana kumezea yale mabaya "tukifanya kazi kwa upendo matokeo yatakuwa mazuri sana, upendo kwa wenzetu haina maana kumezea ya hovyo, kuchukua hatua dhidi ya maovu pia ni upendo"

Aidha, Mhe. Sagini akawataka Watumishi na Viongozi wenzake kumpa ushirikiano ili dhamira ya Rais ya kumpeleka Wizarani hapo iweze kuzaa matunda.

Awali akimkaribisha Naibu Waziri, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alisema yeye na timu nzima ya watumishi wa Wizara wanamtakia majukumu mema na kwamba wako tayari kufanya kazi naye ili kutoa matokeo nyanya kwenda na kasi ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini akiwasili MoCLA*

# Tume Ya Kurekebisha Sheria Jitangazeni Wadau Wawatambue - Sagini



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe Jumanne Sagini akipokelewa katika ofisi za Tume ya Kurekebisha Sheria zilizopo (UDOM) na hatimaye akazungumza na Watumishi wa Taasisi hiyo Mei 8, 2024.*

**Na Hyasinta Kissima**
**- WKS DODOMA**

Akizungumza mara baada ya kutembelea Makao Makuu ya Tume ya Kurekebisha Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora jijini Dodoma, Mei 8, 2024 Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini ameitaka Tume ya Kurekebisha Sheria kujitangaza na kutoa elimu kwa Wadau wa Sheria ili Tume iweze kushiriki ipasavyo katika kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali.

Mhe. Sagini amesema kuwa ipo changamoto ya baadhi ya Wadau wa Sheria kutokujua vizuri majukumu ya Tume na hivyo kuchelewa kuishirikisha Tume katika kufanya mapitio ya Sheria zao.

"Tume ipo kwa mujibu wa Sheria na Katiba yetu na inawajibu wa kufanya tathmini ya Sheria zilizopo kuona zile zilizopitwa na wakati, zinazohitaji marekebisho, utekelezaji wake na changamoto ili kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha Sheria hizo." Alisema Naibu Waziri Sagini.

Kuhusu utekelezaji wa miradi ya Maendeleo, Mhe. sagini amesema kuwa mpaka sasa Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake imeanza kuandika maandiko mbalimbali ili kuweza kuvutia fedha kutoka Serikali au Wadau mbalimbali wa Maendeleo na ameitaka Tume ya Kurekebisha Sheria kushiriki ipasavyo na kutoa mapendekezo yao katika miradi itakayopendekezwa.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu amesema kwa kuwa Tafiti za Kisheria ni sehemu mojawapo ya majukumu ya Tume, ni vyema wakaanzisha mashirikiano na Vyuo mbalimbali vya Elimu ya Juu vyenye kada za Kisheria ili kufanya tafiti nyingi na kupata maarifa zaidi.

***"Toeni elimu kwa Wadau wa Sheria ili Tume iweze kushiriki ipasavyo"***
***Mhe. Sagini***

# MAKONDO ATAKA UMAKINI DAWATI LA HUDUMA ZA KISHERIA



**Na Lusajo Mwakabuku**
**-** WKS DODOMA

Wizara ya Katiba na Sheria imeanzisha Dawati Maalum la huduma za kisheria katika ofisi za wizara hiyo kwa lengo la kutatua kero za wateja wenye malalamiko juu ya huduma za kisheria zinazotolewa katika mifumo mbalimbali ya utoaji haki.

Akizungumza na baadhi ya watumishi Wizarani hapo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Bi. Mary Gasper Makondo alisema dawati hili litarahisisha upatikanaji wa haki kwa wananchi hasa wale wanaofika wizarani kwa ajili ya msaada zaidi.

Aidha Bi. Makondo aliongeza kuwa wananchi wana imani kubwa na serikali hasa kupitia kampeni hii ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia hivyo kila mtumishi ana wajibu wa kuhakikisha kuwa anafanya kazi kwa uadilifu kwa lengo la kuwasaidia wananchi hasa wale wasioukuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili na hatimaye watimize maono ya Rais Samia juu ya wananchi wote kupata haki.

"Wapo watu wana matatizo na wanahangaika kupata msaada

wa kisheria lakini hawajui waanzie wapi, wafanye nini ili kupata huduma hii. Tumeanzisha dawati hili ili mteja atakayefika wizarani aweze kupata huduma bila ya kupoteza muda mrefu kuzunguka maofisini hasa kwa changamoto ambazo nyingi zinahitaji uelewa zaidi. Hivyo hakikisheni mnatoa huduma kiuweledi ili tuweze kuwasaidia wananchi" Alisema Bi. Makondo.

Aidha Katibu Mkuu huyo alitoa rai kwa watumishi wanaowapokea wateja wanaofika wizarani hapo kwa ajili ya huduma kuhakikisha kuwa kuwa wanatumia lugha nzuri, busara na kutoa huduma ndani ya muda mfupi kwani wananchi wengi wanaofika wizarani wanatoka kila pembe ya nchi na wakifika wizarani wanakuwa na tumaini kuwa matatizo yao yatapatiwa ufumbuzi. "Ninapokea wananchi wengi kila siku na wapo wanaotokea maeneo mbali kabisa wanasafiri kwa tabu ila wakiamini kuwa wakifika hapa wizarani wanaamini wameleta changamotozaosehemusahihi.Sasa tunapowahudumia tukumbuke gharama na muda walioutumia mpaka kufika hapa badala ya kuwapa majibu mepesi ambayo hayawasaidii katika changamoto zao." Aliongeza Bi Mary Makondo.

Dawati hili ni muendeleo wa mbinu mbalimbali ambazo Wizara ya Katiba na Sheria imeendelea kuzibuni katika kuhakikisha huduma za kisheria zinawafikia wananchi katika njia rahisi zaidi na zinazopunguza gharama na usumbufu kwa mwananchi.



*Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo (kulia) akikagua nyaraka za mwananchi aliyefika wizarani akitokea Dar es salaam kwa ajili ya kupata msaada zaidi wa kisheria*

# Pongezi..

Viongozi na Watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakitoa zawadi kwa Watumishi wenzao waliopata watoto kwa kipindi cha Januari hadi Machi 2024. Tafrija hiyo fupi ilifanyika katika ukumbi wa mikutano wizarani hapo.



Boadhi ya Viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Watumishi waliopewa zawadi kwa kupata watoto.



Bw. Eric Sezary akikabidhiwa zawadi na Mkurugenzi wa Sera na Mipango Bwana Mbaraka Stambuli.



Mkurugenzi wa Utajiri Asili na Maliasilia DCP Neema Mwanga akimkabidhi zawadi Bw. Alex Toga



Viongozi na Watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria wakiwatakia heri wazazi na watoto katika hafla hiyo.



Bw. Judica Nkya **(Mkali wa hizi kazi)** akitoa neno la shukrani kwa niaba ya watumishi waliopata watoto

# Jukumu la Wananchi Kupata Haki ni Lenu - Waziri Mkuu

**Na William Mabusi**
**-** WKS DODOMA

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) amesema Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria nchini ni jukumu lao kutoa haki kwa wananchi katika kuimarisha misingi ya haki na utawala bora.

Mhe. Majaliwa ametoa kauli hiyo alipokuwa anafungua Mkutano Mkuu wa siku tatu wa Mawakili wa Serikali tarehe 21 Machi, 2024 Jijini Dodoma.

”Serikali inaendela kuchukua hatua za maksudi na madhubuti kuboresha mfumo wa haki jinai, kujenga mazingira wezeshi kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria ya kutoa huduma za kisheria kwa wananchi kote nchini, hivyo ni jukumu lenu kutoa haki kwa wananchi kwa wakati na pasipo kujali dini yake, rangi yake au itikadi ya siasa kwani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania watu wote ni sawa mbele ya sheria na wote wanapashwa kulindwa na kupata haki sawa,” amesema Mhe. Waziri Mkuu.

Akiongelea uhitaji wa huduma ya sheria amesema ”katika miaka ya hivi karibuni jamii imepitia mabadiliko na maendeleo



mbalimbali katika maeneo ya kiuchumi, kiteknolojia, kiasiasa na kiutamaduni. Maendeleo hayo yameongeza uhitaji wa upatinakaji wa huduma za kisheria.”

Akihitimisha hotuba yake Mhe. Majaliwa amewaagiza Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria kutekeleze majukumu yao ya kisheria kwa uadilifu, weledi, uwajibikaji, uaminifu, usiri, umakini na kwa kujituma huku akiwata kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika kutekeleza kampeni ya Msaada wa kisheria ya Mama Samia Lega Aid Campaign kwa kuipa uzito kama majukumu yao mengine ya kila siku.

Aidha, ameziagiza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Taasisi zingine za utoaji haki kufungua na kuimarisha ofisi katika ngazi za chini ili kuhakikisha huduma za kisheria zinawafikia wananchi wengi.

Awali akihutubia kwenye mkutano huo kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana ameyataja matunda ya kazi

wanazofanya Mawakili wa Serikali akisema “katika miaka miwili ya kuwepo kwa Chama cha Mawakili tunashuhudia mchango mkubwa wa Mawakili wa Serikali katika sekta ya sheria ambao umewezesha ustawi wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, uwekezaji, utalii, uhusiano wa kimataifa, utoaji haki, utawala wa sheria, umoja wa kitaifa, na msaada wa kisheria, yote ni matunda ya uwepo wa Mawakili wa Serikali wenye ueledi na ufanisi katika kuchapa kazi.”

Akitaja mafanikio ya miaka mitatu ya Mhe. Rais hususan kwenye sekta ya sheria amesema ”miaka mitatu ya Dkt. Samia tumeona kuundwa kwa Tume ya Haki Jinai ambayo baada ya kazi yake imetoa mapendekezo ya namna ya kuboresha mfumo wa utoaji haki na sasa mapendekezo hayo yameanza kutekelezwa na ofisi nyingi za Serikali,”

Ameyataja mafanikio mengine kuwa ni kuendelea kutolewa kwa msaada wa kisheria kwa wananchi hasa wanyonge kupitia Kampeni ya Kitaifa ya Mama Samia Legal Aid Campaign, hivyo akatoa rai kwa wanasheria kutimiza wajibu wao wa kuwasikiliza watanzania, kwa kuelekeza na kuwasidia kupata huduma ya sheria na hapo watakuwa wameitendea haki Kauli mbiu ya mkutano huo inayosema “Upatikanaji wa huduma za kisheria kwa Wananchi ni nguzo kwa ustawi wa jamii”.

**“katika miaka miwili ya kuwepo kwa Chama cha Mawakili tunashuhudia mchango mkubwa wa Mawakili wa Serikali katika sekta ya sheria”**
**Waziri Mkuu**



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akipokea Miongozo mbalimbali ikiwemo ya Uandishi wa Sheria na Utoaji wa Huduma ya Msaada wa Kisheria iliyozinduliwa wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali, 21 Machi, 2024 Dodoma.*

# AJENDA YA MIRADI YA SERIKALI KUTOZWA KODI KUFIKIKISHWA BUNGENI

**Na Lusajo Mwakabuku**
- WKS DODOMA



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Joseph Mhagama akizungumza wakati wa ziara ya Kamati yake uwandani mkoani Iringa leo 12/03/2024.*

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Joseph Mhagama amesema ni wakati sasa Serikali kuangalia kama kuna tija katika kutoza miradi ambayo inatengenezwa kwa ajili ya wananchi kwani kufanya hivyo si kwamba kunaongeza mlolongo wa utekelezaji wa miradi hiyo peke yake bali pia kunaongeza gharama katika kupitia hatua za upatikanaji wa msamaha wa kodi katika miradi ya Serikali.

Mhe. Mhagama ameyaongea hayo baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Mahakama katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma tarehe 12 Machi, 2024 ikiwa ni sehemu ya ziara ya Kamati hiyo katika kukagua miradi ya maendeleo kwa taasisi zilizo chini ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Mhe. Mhagama alisema kuwa kwake anaona suala hilo halina tija na ni ajenda watakayoenda nayo bungeni kwani tayari hiyo miradi inaandaliwa kwa lengo la kumsaidia mwananchi hivyo hata makusanyo ya kodi hizo ni kwamba mapato yake yanarudi katika kumhudumia mwananchi hivyo ni bora badala ya fedha hizo kurudi hazina zitumike katika kuharakisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

"Kwanza ngoja niwaambie kupatikana kwa msamaha wa kodi ni process, ina mlolongo wake mrefu ambao umesababisha baadhi ya miradi kutoendelea kwa zaidi ya mwaka kusubiria mchakato huo kukamilika. Hela zenyewe zote ni za Serikali ni sawa na kutoa fedha mkono wa kulia kuhamishia mkono wa kushoto. Mbaya zaidi tunachelewasha huduma kwa wananchi wakati wa kufuatilia msamaha hii ya kodi." Alisema Mhe. Mhagama.

Awali akimkaribisha Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Joseph Mhagama na kamati yake, Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwezesha miradi mbalimbali ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria inayolenga kusogeza karibu miundombinu ya utoaji haki kwa wananchi ikiwemo miradi ya ujenzi wa mahakama mbalimbali nchini huku akibainisha kwamba suala hili limeendelea kuongeza imani kwa wananchi kuhusu mahakama ikiwemo matumizi ya teknolojia katika usajili na uendeshaji kesi unaorahisisha kesi nyingi kusikilizwa ndani ya muda mfupi.

Mhe. Chana alisema "kama moja ya jitihada za kupunguza kero kwenye baadhi ya maeneo yenye watu na migogoro mingi mahakama ilikuja na wazo la Mahakama



inyotembea yaani Mobile Court. Kwa jitahada hizo, tumefanikiwa kupunguza mrundikano wa Mashauri hadi kufikia 4%."

Waziri Chana pia akaongeza "Tume ya Kuboresha Haki Jinai imependekeza namna tunavyoweza kuboresha upatikanaji haki kwa masuala ya Jinai ambayo Wizara yetu imeyachukua na inayafanyia kazi ikiwemo matumizi ya TEHAMA kwa upande wa Mahakama kwa mfano mfumo wa mashauri ufahamikao kama Advance Case Management System ambao umeunganishwa na mifumo kadhaa ya wadau, mfumo wa kutafsiri na kutunza kumbukumbu na pia kusikiliza mashauri kwa njia ya Video yaani Video Conference Board."

Mtendaji Mkuu wa Mahakama Prof. Elisante Ole Gabriel akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mahakama alisema "kufanikiwa kwa Mahakama kunatokana na uongozi mzuri wa Jaji Mkuu ambaye ana maono makubwa, lakini pia ushrikiano mkubwa wa mihimili mitatu ndio unaopelekea utekelezaji wa majukumu yetu kuwa rahisi katika kutoa huduma."

"Hadi hivi sasa tumefanikiwa kujenga Mahakama za mwanzo 960 na lengo likiwa ni kufikia Mahakama 3000 nchini kote. Hivi sasa tuna wilaya 139 lakini mahakama zipo 135 zimebakia mahakama 4 tu katika kuhakikisha kila wilaya ina Mahakama nchini. Aidha, katika Ukanda wa Kusini na Mashariki mwa Afrika, Mahakama ya Tanzania ndio inaongoza katika matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki kwa wananchi. Hivi sasa Hakimu anaweza maliza kesi halafu akapata nakala ya kesi ya kurasa 200 chini ya dakika mbili kwa Kiswahili kupitia mfumo wa AI" Alisema Ole Gabriel.

Katika utekelezaji wa miradi hiyo, Mtendaji Mkuu wa Mahakama aliongeza kuwa katika viwango vya ubora wa usimamizi wa miradi ya Mahakama vilivyowekwa na Benki ya Dunia katika miradi yake, Tanzania imefikia asilimia 89 ya ubora wa utekelezaji wa miradi, kiwango ambacho ni cha juu zaidi duniani katika miradi ya Mahakama inayotekelezwa na Benki ya Dunia.

Akielezea changamoto za Wakandarasi katika miradi hiyo, Mtendaji Mkuu wa Mahakama alisema kuna baadhi ya Wakandarasi ambao walipewa kazi nao wakawapa kazi watu wengine na mbaya zaidi wakawa hawana taarifa yeyote juu ya uendelezwaji wa miradi husika suala lililopelekea Mtendaji wa Mahakama kugoma kulipa mpaka suala hilo liwekwe sawa.

Akihitimisha ziara hiyo mkoani Iringa, Mhe. Mhagama alisifia utendaji wa Mahakama na kwamba wao kama kamati ya taasisi hizi wanatembea kifua mbele kutokana na ubunifu, na utekelezaji wa miradi aidha akaiagiza Mahakama kuangalia namna ya kugawanya masurufu katika utekelezaji miradi kwa kuanzia na Tarafa, Majimbo na hatimaye Kata katika kujenga Mahakama.



*Wajumbe wa Kamati pamoja na Watendaji wa Mahakama na viongozi wa Wizara wakipata maelezo Iringa 12/03/2024.*

# Matukio katika Picha



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana kwenye picha ya pamoja na Wajumbe wa Halmashauri ya TUGHE baada kuhutubia Baraza la Wafanyakazi wa Wizara, tarehe 21 Machi, 2024.




Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Watendaji wa Mahakama na viongozi wa Wizara wakiwa katika picha ya pamoja baada ya ziara mkoani Iringa.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akimsikiliza Wakili Onesmo Olengurumwa Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, Mei 07, ofisi za Bunge Dodoma.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko akipokea Tuzo Maalumu ya Ubinadamu aliyotunukiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Maadhimisho ya Miaka 62 ya Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania, Mei 11, 2024 Jijini Dodoma.



Mawakili wa Serikali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria waliokuwa wanashiriki Mkutano Mkuu wa Mawakili wa Serikali baada ya kupiga kura kuwachagua Viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali, tarehe 22 Machi, 2024 Jijini Dodoma.



Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pindi Chana akizungumza na naibu wake Mhe. Jumanne Sagini nje ya kumbi za bunge mara baada ya vikao vya bunge Mei 15, 2024.



Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (mwenye mic), Katibu Mkuu Bi. Mary Makondo, Viongozi wengine wa Wizara na Watumishi wakimpongeza mtumishi mwenzao Dinah Njovu wakati wa sherehe ya harusi yake Aprili 20, 2024.